BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kuendelea kutukarimu neema ya uhai na afya njema sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na pia kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa hali ya amani na utulivu. Aidha, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wawili wa Baraza kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yenu ya kutuongoza katika Baraza wakati tukiendelea kutekeleza wajibu wetu wa kikatiba wa kuidhinisha bajeti kwa niaba ya wananchi wetu ambao tunawawakilisha.

Kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lakoTukufu Maoni ya Kamati ya Uchumi juu ya mchakato mzima wa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa moyo wa dhati napenda kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake mahiri ambao kwa muda mfupi umewajengea imani na matumaini makubwa wananchi wa Zanzibar katika harakati za kujikomboa

na umasikini, kujenga jamii yenye umoja na mshikamano pamoja na kuiletea maendeleo na ustawi nchi yetu ya Zanzibar. Aidha, niwapongeze pia wasaidizi wake wa karibu Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdullah kwa namna wanavyojitolea kwa moyo wao wote katika kumsaidia Mhe. Rais katika kufanikisha malengo ya nchi yetu tuliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatoa shukurani kwa Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa ushirikiano anayoipatia katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Wizara yake licha ya kwamba ameteuliwa hivi karibuni. Kamati pia inatoa pongezi kwa watendaji wa Wizara haswa kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii, Wakurugenzi na watendaji wote wa wizara hiyo kwa ushirikiano wao wanaompa Waziri wao pamoja na Kamati kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda niwapongeze Waheshimiwa Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu kwa juhudi wanazozichukua za kuwawakilisha wananchi wao, juhudi zao zimewawezesha Wananchi kujenga imani kubwa kwa Baraza Lako. Nasi tunawaahidi kwamba tutaendelea kuwatumikia kwa dhati kama ambavyo walivyotuamini kutuchagua na kutuleta katika chombo hiki kwa lengo la kutetea maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni Wajumbe mahiri, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Wajumbe wa Kamati ya Uchumi walifanya kazi kubwa ya kuipitia kwa kina Bajeti ya Fungu L02 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kufanya marekebisho madogo madogo. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo :-

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi kwa karibu sana na makatibu wawili (2) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu, kwa heshima naomba niwatambue:

1. Ndugu Nouman Thabit Nouman – Katibu
2. Ndugu Asma Ali Kassim – Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imefanya kazi ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, siku ya tarehe 21/04/2022, kwa kuzingatia matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa Bajeti inayozingatia program (PBB), Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Fungu Kuu moja la L02 na limepangiwa kutekeleza Programu kuu tatu (3) zenye Programu ndogo sita (6) ambazo kwa ujumla wake zinajumuisha shughuli na huduma zote zinazokusudiwa kutolewa na Wizara hii katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajiwa kukusanya jumla ya Tsh Bilioni 2,259,412,000 kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Aidha, Wizara inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh Bilioni 89,662,400,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Kati ya fedha hizo, Tsh Bilioni 8,107,400,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na Tsh Bilioni 81,555,000,000 ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imesikitishwa na suala la Wizara kuwasilisha taarifa yenye mapungufu mengi kwenye kikao cha kujadili mapendekezo ya bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwenye ngazi ya Kamati. Kwa mfano, Kiambatanisho No. 2 kina mapungufu kwenye asilimia, baadhi ya miradi iliyoainishwa kwenye Kiambatanisho Nam. 4 taarifa zake hazikukamilika, mradi wa ujenzi wa soko la Malindi taarifa ya fedha za wahisani zilizopatikana haikuelezwa ilhali shughuli za ujenzi zinaendelea kwa asilimia 73 wakati Kamati ilipotembelea.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuanzisha na kuendeleza miradi minane (8) ya maendeleo ambapo baadhi ya miradi hiyo inatarajiwa kukamilika hivi karibuni, ukamilikaji wa miradi hiyo itaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi visiwani Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima, sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Uchumi kwa Programu Kuu za Wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea maelekezo na ushauri kama ifuatavyo:

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu hii ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imeundwa na Programu ndogo moja ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu na Huduma nne (4) ambazo zinatekelezwa na Idara ya Maendeleo na Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Pamoja na Mafuta na Gesi). Aidha, lengo kuu la Programu Kuu hii ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu. Programu hii kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, imeombewa jumla ya Tsh Bilioni 14,203,801,000.

Fedha hizo ni ongezeko la Tsh. Bilioni 11,755,801,000 kutoka kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 ambayo ilikuwa ni Tsh. 2,448,000,000. Kamati yangu ilikuwa na shauku ya kujua ni zipi sababu hasa za ongezeko hilo kubwa na kuarifiwa kuwa huduma tatu za kuendeleza sekta ya mafuta na gesi (HL02010102), (HL02010103) na (HL02010104) ndizo zilizokadiriwa kuongeza matumizi hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ndio inayoshughulikia masuala yote ya udhibiti, ufuatiliaji, na uendelezaji wa shughuli za Mafuta na Gesi. Natoa pongezi kwa Wizara kwa kujipanga vizuri katika kuyasimamia masuala yote ya mafuta na gesi kwenye visiwa vyetu, haswa kwa kuwa Serikali kwa kupitia bajeti ya mwaka huu imeongeza fedha za maendeleo kwenye Program hii ya PL0201 hai kufikia Tsh Bilioni 14,203,801,000 ambapo miradi hiyo ya maendeleo itakapokamilika itakuwa ndio chachu ya kufikia malengo yetu ya Zanzibar yenye Uchumi wa bluu. Kamati inashauri kuwepo kwa matumizi mazuri ya fedha hizo ili ziweze kuleta maendeleo kwa wananchi wetu pamoja na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa muda mrefu sasa rasilimali ya mafuta na gesi imekuwa ya kuagizwa kutoka nje ya nchi na biashara hiyo inaathirika kutokana na soko la dunia na kupelekea shughuli za kiuchumi nchini kukosa utulivu wa bei (price stability) kutokana na kupanda na kushuka kwa bidhaa hiyo sokoni (price fluctuation).

Kamati yangu inasisitiza kwa mara nyengine tena suala la kuendelea na utafiti wa utafutaji wa mafuta na gesi. Naiomba Wizara iendelee kufanya Tafiti za kina katika masuala mazima ya Mafuta na Gesi, kwani wananchi wengi wamekua na hamu ya kutaka kujua ni lini hasa rasilimali ya mafuta na gesi itaanza kutoa matunda kwa uchumi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuanza kuwalipa fidia waathirika wa mtetemo licha ya kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazojitokeza ikiwemo suala la baadhi ya waathirika akaunti zao za kibenki kua na hitilafu. Kamati inaitaka Wizara ihaharakishe suala la malipo kwani kadri muda unavyozidi kusonga mbele na thamani ya fedha inazidi kupungua.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi imeundwa na Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari. Programu zote hizi kwa pamoja zinatekelezwa na Idara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mazao ya Baharini pamoja na Idara ya Uhifadhi wa Bahari. Aidha, Programu Kuu hii ina lengo la kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Kupitia program ndogo mbili na huduma kumi na nne, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Programu hii imekadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. Bilioni 2,033,742,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato na kutumia

jumla ya Tsh Bilioni 73,161,643,000 katika kutekeleza shughuli mbalimbali za programu hii.

Kamati yangu inaiomba Wizara kuzitumia fedha hizo kama ilivyopangwa ili kutekeleza kwa ufanisi shughuli za kimaendeleo zilizopangwa kwa ajili ya kuinua pato la wavuvi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kutoa mafunzo kwa wafugaji wa mazao ya baharini kila mwaka ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara imejipangia kutoa elimu kwa wafugaji wa samaki wapatao 200. Tunaiomba Wizara kuendelea kutoa mafunzo kwa vikundi hivi na kuvifikia vikundi vyengine vinavyojishughulisha na uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini ili kuleta tija na kuongeza kipato kwa wananchi wetu. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuchukua juhudi za ziada za kuwasaidia kwenye kutataua changamoto za msingi zinazowakumba wafugaji wa samaki haswa kwenye eneo la kuvua vifaranga vya samaki kwani wafugaji wadogo wamekua wakipoteza vifaranga vingi wakati wa kuvitoa baharini na kuvifikisha kwenye mabwawa. Halikadhalika, Kamati yangu inashauri Wizara kujikita katika kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe faida na fursa zinazotokana na dhana nzima ya Uchumi wa Buluu pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuweza kutatua changamoto wanazokabiliana nazo.

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa jukumu la msingi la Wizara hii ni kuimarisha ulinzi katika maeneo yetu ya bahari kwa kupiga doria za kutosha. Kamati imefurahishwa na mpango wa Wizara wa kununua boti tano za doria kwa mwaka wa fedha 2022/2023,ukilinganisha na mpango wa bajeti ya mwaka 2021/2022 ambapo Wizara ilijipangia kununua boti moja tu idadi ambayo haiendani na kasi ya Uchumi wa buluu.

Aidha, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuwa na mpango wa kuwawezesha wanajamii kuweka matumbawe bandia katika maeneo ya hifadhi za bahari ili kuongeza uzalishaji wa samaki. Pia Kamati inaendelea kuipongeza

Wizara kwa suala la kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii na kuzijengea uwezo kamati za uvuvi 102 Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi na kusimamia rasilimali za bahari kwa kuanzisha maeneo ya ufugaji wa pweza na samaki wa kwenye miamba.

Pia, Kamati inatoa ushauri kwa Wizara kuwafuatilia wale wote waliopata mafunzo hayo yanatolewa zaidi kwa njia ya vitendo na kuwanufaisha wanajamii wenyewe.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuchukua hatua za dharura za kuajiri wakuu wa Madiko katika maeneo mbali mbali nchini ili wasimamiye shughuli za uvuvi kwenye maeneo yao, kutokana na ukweli kwamba kuna upungufu mkubwa wa Wakuu wa madiko hususan kisiwani Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) imeombewa jumla ya shilingi TZS milioni 312,500,000 ikiwa ni Ruzuku ya mishahara kutoka SMZ. Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaipatia ZAFICO jumla ya TZS bilioni 11,000,000,000 kwa kutekeleza mradi wa kutengeza Maboti na kiwanda cha kusarifu samaki na Dagaa kwa ubia na kampuni ya KHAIRU kutoka SRI LANKA. Kamati yangu inatoa pongezi kwa uibuaji wa mradi huo na kuiomba Serikali kupitia Kampuni ya uvuvi (ZAFICO) kutekeleza mradi huo kwa makini ili kuleta tija iliyokusudiwa kwa Taifa letu.

Kadhalika, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Uchumi wa buluu na Uvuvi kwa kupokea boti ya kisasa ya uvuvi (sehewa 03) kutoka nchini SriLanka, pamoja na kuingia ubia na kampuni ya Khairu na kuunda kampuni mpya ya ZAFICO-KHAIRU itakayofanya shughuli za uvuvi wa bahari kuu kwa ujumla wake. Hatua hiyo ni muhimu katika kutia nguvu suala la uvuvi wa bahari kuu nchini na kutatua ile changamoto ya uchache wa utaalamu uliotukabili kwenye boti ya awali ya uvuvi ya (sehewa 02) uliopelekea kuvua

kwa kiwango kidogo, kupotea kwa mitego na kusababisha kukosekana kwa faida kabisa tangu kuanzishwa kwake.

Aidha, Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa kampuni ya ZAFICO kwa kuwaunga wavuvi wadogo wadogo na mikopo ya AMANA Bank ambao wengi wao hawakopesheki moja kwa moja kwa vigezo vya benki. Kamati yangu inashauri wavuvi hao wapewe elimu kabla ya kupatiwa mikopo hiyo ili kufanya matumizi mazuri ya mikopo hiyo na kuwanufaisha wavuvi hao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa jitahada zake za Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 1000 wa samaki na dagaa juu ya njia bora ya kuhifadhi bidhaa hizo Unguja na Pemba na pia Kuwapatia Mashine za boti wavuvi 250 Unguja na Pemba kupitia mkopo wa fedha kutoka CRDB. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha miradi ya maendeleo iliyokusudia kufanya kwa mwaka huu wa fedha kama mradi wa ujenzi wa Kiwanda kitakachojumuisha sehemu ya utengenezaji wa Boti, Uchakataji na usarifu wa samaki Fungu Refu Mkokotoni, mradi wa Ujenzi wa vyumba vya baridi (COLD ROOM) kwa ajili ya kuhifadhia samaki Malindi. Ni dhahiri kuwa huduma hizi ni muhimu na zitawasaidia wananchi kujikwamua kutoka katika janga la umasikini uliokithiri.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya kampuni ya ZAFICO kutaka kujitutumua katika kuendeleza shughuli za uvuvi kibiashara, shughuli zao zimekuwa zikikumbana na changamoto ya gharama za uendeshaji haswa kutokana bei za mafuta ya petroli kuendelea kupanda siku hadi siku hali ambayo inasababisha kushindwa kufikia malengo. Kamati yangu inaomba Serikali iwaondelee kodi kampuni ya ZAFICO kwenye mafuta ili iweze kufikia malengo yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inatambua kuwa Serikali ina nia njema kwenye kulinda

rasilimali zinazopatikana baharini na inatambua kuwa wapo wavuvi na wananchi wanaoishi maeneo ya karibu na bahari ambao wamekuwa wakikiuka sheria na kanuni zilizoekwa. Kutokana na hilo, Kamati yangu inaitaka Serikali kuwashughulikiwa kwa mujibu wa sheria wakosa hao na kuwalinda dhidi ya wale wote watakaojitokeza kuwakandamiza wananchi kupitia jambo hilo. Aidha, Kamati inapendekeza kwenye suala la ulinzi wa fukwe, Wizara Inapaswa ishirikiane na taasisi nyengine zinazohusika na mambo ya mazingira ili kurahisisha kazi hiyo kwani kutokana na mazingira ya visiwa vyetu fukwe ni nyingi na si rahisi kwa taasisi moja peke yake kumudu ulinzi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa ununuzi wa boti 1,077 za aina ya Fiber-Glass kutokana na fedha za ahueni ya UVIKO 19. Kati ya boti hizo, boti 500 ni za wakulima wa mwani, boti 577 ni kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo pamoja na zana zake zinazohusika ikiwemo mashine na vifaa vya kutafutia samaki. Mara baada ya kukamilika ujenzi wa boti hizo zitatolewa kwa wajasiriamali katika vikundi vilivyosajiliwa na kutambulika na kukidhi matakwa ya mkopo huo nafuu kwa nia ya kuwawezesha wananchi haswa wavuvi kujikwamua kwenye wimbi la umasikini.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na

Uvuvi imeundwa na Programu ndogo Tatu zinazojumuisha Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Programu ndogo ya Mipango, Sera na Tafiti na Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Uchumi wa Buluu Afisi Kuu Pemba. Aidha, Programu Kuu hii inatekelezwa na Idara ya Utawala na Uendeshaji na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Lengo la programu hii ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi na ustawi kwa sekta. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 2,296,956,000.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuitanabahisha Wizara kwamba fedha ambazo Baraza lako Tukufu itaziidhinisha kwa Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni fedha za kodi zinazotozwa kutoka kwa Wananchi. Hivyo, Kamati yangu inaitaka Wizara kuwa makini katika matumizi itakayoyafanya ili yale malengo waliyoyapanga yaweze kutekelezwa na Wananchi nao wanufaike ipasavyo kwa mrejesho utakaofanywa kwa matumizi mazuri ya fedha zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano waliotupatia wakati wa kuipitia Bajeti yao. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati yangu imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kuipitia, kuijadili, kutoa mapendekezo yao na hatimae kuiunga mkono na kuipitisha Bajeti hii ili tumuwezeshe Mheshimiwa Waziri kutekeleza yale aliyojipangia katika mwaka ujao wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba ya Kamati yangu ya Uchumi na wananchi wa Jimbo la Kwerekwe, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

…………………………………

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar**.